



## Palipo karibu zaidi kwa mja na Mola wake ni pale anapokuwa kasujudu, Basi zidisheni dua

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake-yakwamba Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Palipo karibu zaidi kwa mja na Mola wake ni pale anapokuwa kasujudu, Basi zidisheni dua".

[Sahih] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Amebainisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- yakuwa mahala palipo karibu zaidi kwa mja na Mola wake ni pale anapokuwa kasujudu; Na hii ni kwa sababu mwenye kusali huweka kiungo bora na kitukufu kuliko vyote katika mwili wake juu ya Ardhi kwa kujinyenyekeza na kujidhalilisha na kunyenyekeka kwa Mwenyezi Mungu -Aliyetakasika na kutukuka- anapokuwa kasujudu. Na ameamrisha -Rehema na amani ziwe juu yake- kukithirisha dua katika sijida, yanakusanyika mambo mawili katika hilo, kujidhalilisha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa kauli na vitendo.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/5382>

النجاة الخيرية  
ALNAJAT CHARITY

